

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA
MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

682


VITENDO VYA KUJIFUNZA HISABATI

Muda: Saa 3

Mwaka: 2022

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A na B zenye jumla ya maswali **kumi na nne (14)**.
2. Jibu maswali yote.
3. Sehemu A in alama **arobaini (40)** na sehemu B ina alama **sitini (60)**.
4. Soma **maelekezo yote** katika kijitabu chako cha kujibia.
5. Vifaa vya mawasiliano na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** katika chumba cha mtihani.
6. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.



SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Kwanini mtoto wa Elimu ya Awali anafundishwa dhana ya kutunza fedha? Fafanua hoja nne kwa kifupi.
2. Nyakati nne za siku hufundishwa kwa watoto wa Elimu ya Awali. Eleza kwa kifupi nyakati hizo.
3. Eleza kwa kifupi vitendo vinne utakavyofanya kumfundisha mtoto wa Elimu ya Awali kutambua majira ya siku katika juma.
4. Zana za kufundishia na kujifunzia tendo la kuongeza na kupunguza vitu zinaweza kupatikana kwa njia mbalimbali. Bainisha njia nne.
5. Ni mambo gani ya kuzingatia katika kufanya upimaji wa maendeleo ya mtoto wa Elimu ya Awali kuhusu stadi za kuongeza na kupunguza vitu? Chambua kwa kifupi mambo manne.
6. Uchaguzi wa mbinu za kufundishia na kujifunzia vitendo vya Hisabati kwa mtoto wa Elimu ya Awali unazingatia mambo mbalimbali. Fafanua kwa kifupi mambo manne.
7. Je, vifaa vifuatavyo hutumikaje katika maisha ya kila siku?
(a) Mizani (b) Futi kamba
(c) Saa (d) Rula.
8. Kwa nini ni muhimu kwa mwalimu kutumia andalia la somo la Hisabati wakati anapofundisha darasani? Taja hoja nne kwa ufupi.
9. Eleza kwa kifupi changamoto nne unazoweza kukumbana nazo kwa kuwaruhusu watoto kwenda kukusanya zana za kujifunzia na kufundishia katika mazingira yanayozunguka shule.
10. Upimaji wa maendeleo ya mtoto katika somo la Hisabati una faida gani? Toa hoja nne.

SEHEMU B (Alama 60)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

11. Kwa kutumia hoja tano, eleza jinsi utakavyomfundisha mtoto wa Elimu ya Awali ili aweze kuongeza vitu vyenye jumla isiyozidi 10 kwa usahihi.
12. Eleza vitendo vitano atakavyofanya mwalimu kumfundisha mtoto wa Elimu ya Awali dhana ya kupunguza vitu visivyozidi 10.

13. Kwa kutumia swali linalomuuliza mwanafunzi; “3 ongeza 4 ni sawa na ngapi?” fafanua hatua nne ambazo mwalimu atazingatia wakati wa kumfundisha mtoto kupata jibu la swali hilo.
14. Eleza hatua tano za andalio la somo la kufundishia Hisabati katika ngazi ya Elimu ya Awali.